

UBORA WA UISLAMU

Muhammad bin Abdul-Wahhab

Kitabu hiki kilicho tafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili, kinazungumzia: Maana ya uislamu, ubora wa uislamu na uwajibu wa kuingia katika uislamu.

<https://islamhouse.com/818735>

- [Ubora Wa Uislamu](#)
- -
 - [1. Utukufu wa Uislamu](#)
 - [2. Uwajibu wa kuingia katika Uislamu](#)
 - [3. Maana ya Uislamu](#)
- -

- 4. Na yejote anayetaka dini
isiyokuwa ya Kiislamu basi
haitokubaliwa kwake
- 5. Ni wajibu kufuata Qur-aan
peke yake
- 6. Hakuna manasibisho
yasiyokuwa ya Kiislamu
- 7. Uwajibu wa kujisalimisha
kikamilifu na kuacha mengine
yote
- 8. Bid'ah ni mbaya zaidi
kuliko madhambi makubwa
- 9. Allaah ameizuia tawbah
kwa mtu wa Bid'ah

- 10. Watu wa Kitabu ni kwanini mnahojiana kuhusu Ibraahiyim?
- 11. Elekeza uso wako katika Dini yenye imani safi na iliyotakasika
- 12. Ugeni wa Uislamu na ubora wa wagoni
- 13. Matahadharisho ya Bid'ah

ora Wa ﴿

Ubora Wa Uislamu

Mwandishi:

Imaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab

Tarjama:

Abu Bakr Khatwiyb al-Atrush

1. Utukufu wa Uislamu

Allaah (Ta'ala) amesema:

الْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَنْمَطْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيَتُ لَكُمُ الْإِسْلَامَ دِيَنًا

"Leo Nimekukamilishieni Dini yenu na Nime kutimizieni neema Yangu na Nimekuridhieni kwenu Uislamu uwe [ndio] Dini yenu." (05:03)

فَلْ يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنْ كُنْتُمْ فِي شَكٍّ مِّنْ دِينِي فَلَا أَعْبُدُ الَّذِينَ تَعْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ وَلَكِنْ أَعْبُدُ اللَّهَ الَّذِي يَتَوَفَّ أَكُمْ

"Sema: “Enyi watu! Ikiwa mna shaka kutokana na Dini yangu, basi [mimi] siabudu ambavyo mnaviabudu badala ya Allaah; lakini namwabudu Allaah Ambaye [siku moja] Atakufisheni.”

(10:104)

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِذْ قَرَأُوا الْكِتَابَ وَآمَنُوا بِرَسُولِهِ يُؤْتُكُمْ كَفَلَيْنِ مِنْ رَحْمَتِهِ وَيَجْعَلُ لَكُمْ نُورًا تَمْشُونَ بِهِ
وَبِغُفرَانٍ لَكُمْ ۝ وَاللَّهُ عَفُورٌ رَّحِيمٌ

"Enyi mliaoamini! Mcheni Allaah na muaminini Mtume Wake! Hapo Atakupeni sehemu mbili kati ya Rahmah Zake na Atakujaalieni Nuru mnatembea nayo na Akusameheeni - Allaah ni Ghafuwrur-Rahiym, Mwingi wa kusamehe, Mwenye kurehemu."
(57:28)

al-Bukhaariy amepokea kupitia kwa Ibn 'Umar (**Radhiya Allaahu 'anhuma**) ya kwamba Mtume wa Allaah (**Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam**) amesema:

"Mfano wenu nyinyi na watu wa Kitabu ni kama mfano mtu mwenye

kukodisha wafanyakazi na akasema:
"Ni nani katika nyinyi anayetaka
kunifanyiakazi kuanzia asubuhi mpaka
mchana kwa senti moja?" Mayahudi
wakafanya hivo. **Halafu akasema:** "Ni
nani katika nyinyi anayetaka
kunifanyia kazi kuanzia mchana
mpaka 'Aswr kwa senti moja?"
Manaswara wakafanya hivo. **Kisha
akasema:** "Ni nani katika nyinyi
anayetaka kunifanyiakazi
kuanzia 'Aswr mpaka jua kuzama kwa
senti mbili?" Ndio nyinyi. **Mayahudi
na manaswara wakakasirika na
kusema:** "Ni kwa nini sisi ndio tufanye
kazi sana na kupata ujira mdogo?"
Akasema: "Nimepunguza kitu katika
haki yenu?" Wakasema: "Hapana."

Ndipo akasema: "Hiyo ni fadhila yangu ninampa yule ninayemtaka."[\[1\]](#)

al-Bukhaariy amepokea kuitia kwa Abu Hurayrah (**Radhiya Allaahu 'anh**) ya kwamba Mtume wa Allaah (**Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam**) amesema:

"Allaah amewapoteza waliokuwa kabla yetu siku ya ijumlaha. Mayahudi wakapata jumamosi na manaswara jumapili. Allaah akatuleta na akatuongoza siku ya ijumlaha. Kadhalika watatufuata siku ya Qiyaamah. Sisi ndio wa mwisho katika dunia hii, wa kwanza siku ya Qiyaamah."[\[2\]](#)

al-Bukhaariy amepokea kwa mlolongo wa wapokezi wenye kupungua

kwamba Mtume (**Swalla Allaahu `alayhi wa sallam**) amesema:

"Dini yenyewe kupendwa zaidi na Allaah ni ule upwekeshaji mwepesi."[\[3\]](#)

Ubayy bin Ka'b (**Radhiya Allaahu `anh**) amesema:

"Shikamaneni na Njia na Sunnah. Hakuna mja mwenye kushikamana na Njia na Sunnah akamfikiria Allaah mpaka macho yake yakatiririka machozi kwa kumwogopa Allaah kisha aunguzwe na Moto. Hakuna mja mwenye kushikamana na Njia na Sunnah akamfikiria Allaah mpaka mwili wake ukasisimka kwa kumwogopa Allaah isipokuwa mfano wake ni kama mfano wa jani kavu

kwenye mti lenye kuruka hewani; hali kadhalika yanamtoka madhambi yake. Ni bora kuwa mwenye kujizuia katika Njia na Sunnah kuliko kuwa na bidii katika yanayokwenda kinyume na Njia na Sunnah."[\[4\]](#)

Abud-Dardaa' (Radhiya Allaahu 'anh) amesema:

"Kule wale wenye busara wakawa ni wenye kulala na kuacha kufunga ni bora kuliko wajinga kuswali usiku na kufunga. Chembe kidogo ya wema ilio pamoja na uchaMungu na yakini, ni bora na ni yenyewe uzito kuliko 'ibaadah za waliodanganyika zilizo kubwa sawa na mlima."[\[5\]](#)

2. Uwajibu wa kuingia katika Uislamu

Allaah (Ta'ala) amesema:

وَمَنْ يَتَّبِعْ غَيْرَ الْإِسْلَامِ بَيْنَا فَلَنْ يُفْلِحْ مِنْهُ وَهُوَ فِي الْآخِرَةِ مِنَ الْخَاسِرِينَ

"Na yejote anayetaka dini isiyokuwa ya Kiislamu basi haitokubaliwa kwake, naye katika Aakhirah atakuwa mionganini mwa waliokhasirika."

(03:85)

إِنَّ الَّذِينَ عِنْدَ اللَّهِ إِلَيْهِ الْأَسْلَامُ

"Hakika Dini mbele ya Allaah ni Uislamu." (03:19)

وَأَنَّ هَذَا صِرَاطِي مُسْتَقِيمًا فَلَا تَبْغِعُوهُ ۝ وَلَا تَنْتَهُوا السُّبُلَ فَقَرَّقَ بِكُمْ عَنْ سَبِيلِهِ

“Hii ndio njia Yangu, [njia] iliyonyooka; basi ifuatani na wala msifuate vichochoro [vinginevyo]; vikakufarikisheni na njia Yake!”

(06:153)

Mujaahid amesema:

"Vichochoro ni Bid'ah na utata."

‘Aaishah (Radhiya Allaahu ‘anhaa) amesema kuwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) amesema:

"Mwenye kuzusha katika amri yetu hii yasiyokuwemo yatarudishwa."[\[6\]](#)

Ameipokea al-Bukhaariy na Muslim.

Katika upokezi mwingine imekuja:

"Mwenye kufanya tendo lisiloafikiana na amri yetu litarudishwa."[\[7\]](#)

al-Bukhaariy amepokea kupitia kwa Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu ‘anh)

ya kwamba Mtume wa Allaah (**Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam**) amesema:

"Ummah wangu wote utaingia Peponi isipokuwa yule asiyetaka." **Wakasema:** "Ee Mtume wa Allaah! Ni nani atayekataa?" Akasema: "Mwenye kunitii ataingia Peponi na mwenye kuniasi amekataa." [\[8\]](#)

al-Bukhaariy amepokea kupitia kwa Ibn 'Abbaas (**Radhiya Allaahu 'anhuma**) ya kwamba Mtume wa Allaah (**Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam**) amesema:

"Watu wanaochukiwa zaidi na Allaah ni watatu; mtenda dhambi Haram, mwenye kutaka katika Uislamu kitu cha Jaahiliyyah na mwenye kuomba

damu ya mtu muislamu pasina haki ili amwage damu yake."[\[9\]](#)

Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah
(Rahimahu Allaah) amesema:

"Kitu cha Jaahiliyyah inahusu kila kitu cha Jaahiliyyah, isiyofungwa [mutlaq] au iliyofungwa [muqayyad] kwa mtu kama myahudi, mnaswara, mwabudu sanamu au mwingine mwenye kwenda kinyume na yale waliyokuja nayo Mitume."

al-Bukhaariy amepokea kutoka kwa Hudhayfah ambaye amesema:

"Enyi wanazuoni! Bakieni katika njia iliyonyooka! Mkifanya hivo basi mmetangulia mbele. Na mkienda

kuliani na kushotoni basi mmepotea upotevu wa mbali kabisa."[\[10\]](#)

Muhammad bin Wadhdhwaah ameелеza jinsi Hudhayfah alivyokuwa akiingia msikitini na kusema haya.

[Akasema:](#)

"Sufyaan bin 'Uyaynah ametueleza, kutoka kwa Mujaalid bin Sa'iyd, kutoka kwa 'Aamir ash-Sha'biiy, kutoka kwa Masruuq ambaye ameèleza kuwa 'Abdullaah bin Mas'uud (*Radhiya Allaahu 'anh*) amesema:

"Hakuna mwaka unaokuja isipokuwa ulio baada yake ni mbaya zaidi. Simaanishi kuwa kuna mwaka wenye kunyesha zaidi kuliko mwingine au wenye rutuba zaidi kuliko mwingine

wala kiongozi ambaye ni bora kuliko mwingine. Ninachomaanisha ni kwenda kwa wanazuoni wenu na watu wenu bora. Kisha kutajitokeza watu ambao watayakisia mambo kwa matamanio yao ambapo watauharibu Uislamu na uangamie."[\[11\]](#)

3. Maana ya Uislamu

Allaah (**Ta’ala**) amesema:

فَإِنْ حَاجُوكَ فَقْلَ أَسْلَمْتُ وَجْهِي لِلَّهِ وَمَنْ اتَّبَعَنِ

"Na wakikuhoji, **basi sema:**

“Nimejisalimisha kwa Allaah
kikamilifu na wale walionifuata.”
(03:20)

al-Bukhaariy na Muslim wamepokea
kupitia kwa Ibn ‘Umar (**Radhiya
Allaahu ‘anhuma**) ya kwamba Mtume

wa Allaah (*Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam*) amesema:

"Uislamu ni kushuhudia ya kwamba hapana mola mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allaah na kwamba Muhammad ni Mtume wa Allaah, kusimamisha swalah, kutoa zakaah, kufunga Ramadhaan na kuhiji kwenye Nyumba ukiweza kuiendea."[\[12\]](#)

al-Bukhaariy na Muslim wamepokea kupitia kwa Abu Hurayrah (*Radhiya Allaahu 'anh*) ya kwamba Mtume wa Allaah (*Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam*) amesema:

"Muislamu ni yule mwenye
kuwasalimisha waislamu kwa ulimi na
mkono wake."[\[13\]](#)

Bahz bin Hakiyam amepokea kutoka
kwa baba yake, kutoka kwa babu yake
ambaye ameeleza kuwa alimuuliza
Mtume wa Allaah (**Swalla Allaahu
`alayhi wa sallam**) juu ya Uislamu
ambapo akajibu:

"Ni kuusalimisha moyo wako kwa
Allaah (**Ta`ala**), kuuelekeza uso wako
kwa Allaah (**Ta`ala**), kuswali swalah
za faradhi na kutoa zakaah
iliyofaradhishwa."[\[14\]](#)

Ameipokea Ahmad.

Abu Qilaabah amepokea kutoka kwa mtu miongoni mwa watu wa Shaam ambaye amepokea kutoka kwa baba yake ambaye alimuuliza Mtume wa Allaah (**Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam**) kuhusu Uislamu ambapo akajibu:

"Ni kuusalimisha moyo wako kwa Allaah (**Ta'ala**) na waislamu wasalimike na ulimi na mkono wako."

Akasema: "Ni Uislamu upi bora?"

Akajibu: "Imani." **Akauliza:** "Ni nini imani?" Akajibu: "Ni kumwamini Allaah, Malaika Wake, Vitabu Vyake, Mitume Wake na kufufuliwa baada ya kufa." [**\[15\]**](#)

4. Na yevote anayetaka dini isiyokuwa ya Kiislamu basi haitokubaliwa kwake

Abu Hurayrah (**Radhiya Allaahu 'anh**) ameeleza kuwa Mtume wa Allaah (**Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam**) amesema:

"Matendo yatakuja siku ya Qiyaamah. **Swalah itakuja na kusema:** "Ee Mola! Mimi ndio swalah." **Aseme:** "Uko katika kheri." **Kisha ije swadaqah na kusema:** "Ee Mola! Mimi ndio swadaqah." **Aseme:** "Uko katika kheri." **Kisha ije swawm na kusema:** "Ee Mola! Mimi ndio swawm." **Aseme:** "Uko katika kheri." Halafu yaje matendo mengine yote na Aseme:

"Uko katika kheri." **Kusha kuje Uislamu na kusema:** "Ee Mola! Wewe ni as-Salaam na mimi ndio Uislamu."
Aseme: "Uko katika kheri." Leo hii Nitachukua na Kupeana kutokana na wewe." Allaah (**Ta'ala**) amesema:

وَمَنْ يَبْتَغِ غَيْرَ الْإِسْلَامِ فَلَأَنَّ يُقْبَلَ مِنْهُ وَهُوَ فِي الْآخِرَةِ مِنَ الْخَاسِرِينَ

"Na yejote anayetaka dini isiyokuwa ya Kiislamu basi haitokubaliwa kwake, naye katika Aakhirah atakuwa miongoni mwa waliokhasirika."
(03:85)

Kumepokelewa [Hadiyth] Swahiyh ya kwamba 'Aaishah (**Radhiya Allaahu 'anhaa**) ameeleza kuwa Mtume wa (**Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam**) amesema:

"Mwenye kufanya tendo lisiloafikiana na amri yetu litarudishwa."

Ameipokea Ahmad.

-

5. Ni wajibu kufuata Qur-aan peke yake

Allaah (Ta'ala) amesema:

وَنَزَّلْنَا عَلَيْكَ الْكِتَابَ تِبْيَانًا لِكُلِّ شَيْءٍ

"Na Tumekuteremshia Kitabu kikiwa ni kielezo bayana cha kila kitu."

(16:89)

an-Nasaa'iy na wengine wamepokea ya kwamba Mtume (**Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam**) aliona kwenye mikono ya 'Umar bin al-Khattaab

(Radhiya Allaahu 'anh) karatasi ya Tawrat akasema:

"Ee mwana wa al-Khattwaab! Una shaka? Nimekufikishieni wazi wazi kabisa. Lau Muusa angelikuwa hai hii leo mkamfuata badala ya kunifuata mimi basi mgelikuwa mmepotea."

'Umar akasema: "Nimeridhia Allaah kuwa Mola Wangu, Uislamu kuwa dini yangu na Muhammad kuwa Mtume wangu."[16]

Katika upokezi mwingine imekuja:

"Lau Muusa angelikuwa hai hii leo asingelikuwa na namna isipokuwa kunifuata."

6. Hakuna manasibisho yasiyokuwa ya Kiislamu

Allaah (Ta'ala) amesema:

هُوَ سَمَّاْكُمُ الْمُسْلِمِينَ مِنْ قَبْلٍ وَفِي هَذَا

"Yeye Ndiye hapo kabla [katika Vitabu vya awali] na katika [Kitabu] hiki Aliyekuiteni "Waislamu"."
"(22:78)

al-Haarith al-Ash'ariy (**Radhiya Allaahu 'anh**) ameeleza kuwa Mtume (**Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam**) amesema:

"Ninakuamrishi ni mambo matano ambayo Allaah ameniamrisha kwayo; usikivu, utiifu, Jihaad, Hijrah na mkusanyiko, Jamaa'ah. Hakika mwenye kuacha mkusanyiko kiasi cha shibri basi amevua kamba ya Uislamu

katika shingo yake isipokuwa ikiwa kama atajirudi. Mwenye kuita wito wa Jaahiliyyah ataadhibiwa Motoni." **Mtu mmoja akasema:** "Ee Mtume wa Allaah! Hata kama ataswali na kufunga?" Akajibu: "Hata kama ataswali na kufunga. Enyi waja wa Allaah! Iteni kwa wito wa Allaah; Yeye ndiye kakwiteni "waislamu" na "waumini"."[\[17\]](#)

Ameipokea Ahmad na at-**Tirmidhiy ambaye amesema:**

"Hadiyth ni Hasan na Swahiyh."

Kumepokelewa [Hadiyth] Swahiyh ya kwamba Mtume (**Swalla Allaahu `alayhi wa sallam**) amesema:

"Mwenye kuacha mkusanyiko kiasi cha shibri na akafa, amekufa kifo cha Jaahiliyyah."

Mtume (**Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam**) amesema pia:

"Mnaita wito wa Jaahiliyyah ilihali niko kati yenu?"

Abul-'Abbaas amesema:

"Kila jina lenye kwenda kinyume na Uislamu na Qur-aan na manasibisho ya nasabu, miji, makabila, madhehebu au mifumo ni katika sifa za Jaahiliyyah. Pindi mtu wa Muhaajiruun alipozozana na mtu wa Answaar na kila mmoja akawaita watu wake, ndipo Mtume

(Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam)
akasema:

"Mnaita wito wa Jaahiliyyah ilihali
niko kati yenu?"

Akaghadhibika sana kutokana na
hilo."[\[18\]](#)

-

7. Uwajibu wa kujisalimisha kikamilifu na kuacha mengine yote

Allaah (Tabaarak wa Ta'ala) amesema:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا ادْخُلُوا فِي السَّلَامِ كَافَةً وَلَا تُنْتَجِعُوا خُطُواتِ الشَّيْطَانِ ۝ إِنَّهُ لَكُمْ عَذُونٌ مُّبِينٌ

"Enyi mlionamini! Jisalimisheni
kikamilifu na wala msifuate hatua za
Shaytwaan - hakika yeye kwenu ni
adui wa wazi." (02:208)

أَلْمَ تَرَ إِلَى الَّذِينَ يَرْعُمُونَ أَنَّهُمْ آمَنُوا بِمَا أَنْزَلَ إِلَيْكُمْ وَمَا أَنْزَلَ مِنْ قَبْلِكُمْ يُرِيدُونَ أَنْ يَتَحَكَّمُوا إِلَيْ

الطَّاغُوتِ وَقَدْ أَمْرُوا أَن يَكْفُرُوا بِهِ وَيُرِيدُ الشَّيْطَانُ أَن يُضْلِلُهُمْ ضَلَالًا بَعِيدًا

"Je, huoni wale wanaodai kwamba wao
wameamini yaliyoteremshwa kwako
na yale yaliyoteremshwa kabla yako,
jinsi wanataka wahukumiane
kwa hukumu za kufuru na hali
wameamrishwa wazikanushe? Na
Shaytwaan anataka awapoteze upotofu
wa mbali." (04.60)

إِنَّ الَّذِينَ فَرَّقُوا بَيْنَهُمْ وَكَانُوا شَيْعًا لَسْتَ مِنْهُمْ فِي شَيْءٍ ۝ إِنَّمَا أَمْرُهُمْ إِلَى اللَّهِ ثُمَّ يُنَبِّئُهُمْ بِمَا كَانُوا
يَفْعَلُونَ

"Hakika wale waliofarikisha dini yao
na wakawa makundi makundi huna
lolote kuhusiana na wao. Hakika amri
yao iko kwa Allaah, kisha
Atawajulisha kwa yale waliyokuwa
wakifanya." (06:159)

يَوْمَ تَبَيَّضُ وُجُوهٌ وَتَسْوُدُ وُجُوهٌ ۝ فَإِنَّمَا الَّذِينَ اسْوَدَتْ وُجُوهُهُمْ أَكَفَرُهُمْ بَعْدَ إِيمَانِهِمْ فَذُوقُوا الْعَذَابَ
بِمَا كُنْتُمْ تَكْفُرُونَ

"Siku [baadhi ya] nyuso zitang'ara na

[nyingine] zitafifia. Basi wale ambao nyuso zao zitafifia [wataambiwa:] “Je, mlikufuru baada ya kuamini kwenu? Basi onjeni adhabu kwa yale mliyokuwa mkikufuru.” (03:106)

Ibn ‘Abbaas (*Radhiya Allaahu ‘anhumaa*) amesema:

“Wale walioshikamana na Sunnah na mshikamano ndio nyuso zao zitang’ara na wale walioshikamana na Bid’ah na tofauti ndio nyuso zao zitafifia.” [\[19\]](#)

‘Abdullaah bin ‘Amr (*Radhiya Allaahu ‘anhumaa*) ameeleza kuwa Mtume wa Allaah (*Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam*) amesema:

"Ummah wangu utafikwa na yale yaliyowafika wana wa Israaiyl kiasi cha kwamba, ikiwa kuna katika wao aliyemwingilia mama yake hadharani basi kutapatikana katika Ummah wangu ambaye atafanya vivyo hivyo. Wana wa Israaiyl walifarikiana katika makundi sabini na mbili na Ummah wangu utafarikiana katika makundi sabini na tatu; yote yataingia Motoni isipokuwa moja tu." **Wakasema:** "Ee Mtume wa Allaah! Ni lipi hilo?" Akasema: "Ni lile linalofuata yale mimi na Maswahabah zangu tunayofuata."[\[20\]](#)

Muumini ambaye anataraji kukutana na Allaah azingatie maneno ya mkweli

na msadikishwaji na khaswa pale
aliposema:

"Ni lile linalofuata yale mimi na
Maswahabah zangu tunayofuata."

Ni mawaidha yaliyoje lau yatazifikia
nyoyo zilizo hai!"

Ameipokea at-Tirmidhiy.

at-Tirmidhiy ameipokea tena kupitia
kwa Abu Hurayrah na akaisahihisha.
Lakini hata hivyo ndani yake
hakukutajwa Moto, kama ilivyo katika
Hadiyth ya Mu'aawiyah inayopatikana
kwa Ahmad na Abu Daawiud. **Humo**
mna:

"Kutajitokeza watu katika Ummah
wangu ambao watachukua matamanio

hayo kama jinsi mbwa kichaa inavyomuathiri muathirikaji; haitoacha mshipa wala kiungo isipokuwa itaingia ndani yake."[\[21\]](#)

Tafsiri ya maneno ya Mtume (**Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam**) "mwenye kutaka katika Uislamu kitu cha Jaahiliyyah" imeshatangulia.

-

8. Bid'ah ni mbaya zaidi kuliko madhambi makubwa

Allaah ('Azza wa Jall) amesema:

إِنَّ اللَّهَ لَا يَعْفُرُ أَن يُشْرَكَ بِهِ وَيَعْفُرُ مَا دُونَ ذَلِكَ لِمَن يَشَاءُ ۝ وَمَن يُشْرِكُ بِاللَّهِ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَالًا بَعِيدًا

"Hakika Allaah Hasamehi kushirikishwa; lakini Anasamehe

yasiyokuwa hayo kwa Amtakae; na
yejote atakayemshirikisha Allaah basi
kwa yakini amepotoka upotofu wa
mbali." (04:116)

فَمَنْ أَظْلَمَ مِنْ أَفْرَىٰ عَلَىٰ اللَّهِ كَيْبَا لِيُضِلَّ النَّاسَ بِغَيْرِ عِلْمٍ ۝ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الظَّالِمِينَ

"Ni nani dhalimu zaidi kuliko yute
anayemtungia Allaah uongo ili apoteze
watu bila elimu? Hakika Allaah
Hawaongozi watu madhalimu."

(06:144)

لِيَحْمِلُوا أُوزَارَهُمْ كَامِلَةً يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۝ وَمَنْ أُوزَارَ الدِّينَ يُضْلَوْنَهُمْ بِغَيْرِ عِلْمٍ ۝ أَلَا سَاءَ مَا
يَرْزُونَ

"Ili wabebe mizigo [ya madhambi] yao
kamili Siku ya Qiyaamah na mizigo ya
wale waliowapoteza bila ya elimu.
Tanabahi! Uovu ulioje
wanayoyabeba." (16:25)

al-Bukhaariy na Muslim wamepokea
ya kwamba Mtume (Swalla Allaahu

‘alayhi wa sallam) amesema kuhusu Khawaarij:

"Popote mnapokutana nao waueni. Ikiwa nitakutana nao basi nitawaua kama walivyouawa kina ‘Aad."[\[22\]](#)

Kumepokelewa [Hadiyth] Swahiyh ya kwamba Mtume (**Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam**) amekataza kupambana na viongozi madhalimu maadamu [wanaswali](#)[\[23\]](#).

Jariyr bin ‘Abdillaah (**Radhiya Allaahu ‘anhumaa**) ameeleza kuwa kuna mtu aliyetoa swadaqah na watu wakawa wamemuiga. Mtume wa Allaah (**Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam**) akasema:

"Yule mwenye kuanzisha katika Uislamu msingi mzuri basi ana ujira wake na ujira wa yule atakayeifanya baada yake pasina kupungua chochote katika ujira wao. Na yule mwenye kuanzisha katika Uislamu msingi mbaya basi ana madhambi yake na madhambi na yule atakayeifanya pasina kupungua chochote katika madhambi yao."[\[24\]](#)

Ameipokea Muslim ambaye amepokea tena mfano wa Hadiyth kama hiyo kupitia kwa Abu Hurayrah:

"Yule mwenye kuita katika uongofu..." na "Yule mwenye kuita katika upotevu..."[\[25\]](#)

9. Allaah ameizuia tawbah kwa mtu wa Bid'ah

Yamepokelewa katika Hadiyth ya Anas bin Maalik pamoja na al-Hasan al-Baswriy kwa mfuatano wa wasimulizi uliokatika kutoka kwa Mtume (**Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam**). Ibn Wadhdhwaah ameeleza kuwa Ayyuub amesema:

"Kuna mtu katika sisi aliyekuwa na I'tiqaad mbovu na baadae akaiacha. **Nikamwendea Muhammad bin Siriyn** na kumwambia: "Je, unajua kuwa fulani ameacha I'tiqaad yake?" Akasema: "Tazama amegeuka kuwa nini. **Sehemu ya mwisho ya Hadiyth ni**

kipigo kwao kuliko sehemu yake ya mwanzo:

"Wanatoka katika Uislamu na kisha hawarudi tena." [\[26\]](#)

Ahmad bin Hanbal aliulizwa maana yake akajibu:

"Hawawafikishwi tawbah."

10. Watu wa Kitabu ni kwanini mnahojiana kuhusu Ibraahiyim?

Allaah (Ta'ala) amesema:

يَا أَهْلَ الْكِتَابِ لَمْ تُحَاجُونَ فِي إِبْرَاهِيمَ وَمَا أَنْزَلْتَ النَّوْرَةَ وَالْإِنْجِيلَ إِلَّا مِنْ بَعْدِهِ ۝ أَفَلَا تَعْقِلُونَ هَا أَنْتُمْ هُؤُلَاءِ حَاجِنُمْ فِيمَا لَمْ يَهِ عِلْمٌ فَلِمْ تُحَاجُونَ فِيمَا لَيْسَ لَكُمْ بِهِ عِلْمٌ ۝ وَاللَّهُ يَعْلَمُ وَأَنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ مَا كَانَ إِبْرَاهِيمُ يَهُوَدِيًّا وَلَا نَصْرَانِيًّا وَلَكِنْ كَانَ حَنِيفًا مُسْلِمًا وَمَا كَانَ مِنَ الْمُشْرِكِينَ

"Enyi watu wa Kitabu! Kwanini

mnahojiana kuhusu Ibraahiyim na hali haikuteremshwa Tawraat na Injiyl isipokuwa baada yake? Je, hamtii akilini? Nyinyi ndio hawa mlionhojiana katika yale ambayo mnayo elimu nayo, basi kwa nini [sasa] mnahojiana katika yale msiyokuwa na elimu nayo? Na Allaah Anajua, na nyinyi hamjui. Hakuwa Ibraahiyim yahudi wala naswara - lakini alikuwa ni mwenye imani iliyo safi na kutakasika na alikuwa ni Muislamu; na hakuwa miongoni mwa washirikna." (03:65-67)

وَمَنْ يَرْغُبُ عَنْ مَلَأِ إِبْرَاهِيمَ إِلَّا مَنْ سَفِهَ نَفْسَهُ ۝ وَلَقَدِ اصْطَفَيْنَا فِي الدُّنْيَا ۝ وَإِنَّهُ فِي الْآخِرَةِ لِمِنَ الصَّالِحِينَ

"Na nani atakayejitenga na imani ya Ibraahiyim isipokuwa anayeitia nafsi yake upumbavu? Na kwa yakini

Tumemchagua duniani, naye Aakhirah ni mionganii mwa [waja] wema."
(02:130)

Hadiyth kuhusu Khawaarij imeshatangulia. al-Bukhaariy na Muslim wamepokea ya kwamba Mtume (**Swalla Allaahu `alayhi wa sallam**) amesema:

"Kizazi cha baba fulani sio mawalii wangu. Mawalii wangu ni wale wachaMungu." [\[27\]](#)

al-Bukhaariy na Muslim wamepokea kupitia kwa Anas ya kwamba Mtume wa Allaah (**Swalla Allaahu `alayhi wa sallam**) alipata khabari kuwa kuna Maswahabah waliosema: "Mimi sintokula nyama." **Mwingine** akasema:

"Nitaswali tu na sintolala." **Mwingine** akasema: "Mimi sintooa." **Mwingine** akasema: "Nitafunga tu." Mtume (**Swalla Allaahu `alayhi wa sallam**) akasema:

"Mimi ninaswali na kulala, ninafunga na kuacha, ninaoa na kula nyama. Atakayeipa mgongo Sunnah yangu basi huyo si katika mimi." [\[28\]](#)

Tafakari ni ukali namna gani Mtume (**Swalla Allaahu `alayhi wa sallam**) alivyowakemea baadhi ya Maswahabah pindi walipotaka kuishi maisha ya kuipa nyongo dunia kwa kupitiliza ili kumuabudu Allaah na akaita matendo yao kuwa ni kuipa mgongo Sunnah yake. Unafikiriaje

inapokuja katika Bid'ah nyinginezo?
Unafikiriaje inapokuja kwa wengine
wasiokuwa Maswahabah?

-

11. Elekeza uso wako katika Dini yenye imani safi na iliyotakasika

Allaah (Ta'ala) amesema:

فَأَقِمْ وَجْهَكَ لِلَّذِينَ حَنِيفُوا فَطَرَ اللَّهُ الَّتِي فَطَرَ النَّاسَ عَلَيْهَا لَا تَبْدِيلَ لِخَلْقِ اللَّهِ ذَلِكَ
الَّذِينَ الْقَوِيمُونَ وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ

"Basi elekeza uso wako katika Dini
yenye imani safi na iliyotakasika,
imani hiyo ndio maumbile Allaah
Aliyowaumbia watu [wote] - hakuna
mabadiliko katika uumbaji wa Allaah!
Hivyo ndio Dini iliyonyooka
sawasawa, lakini watu wengi hawajui.
(30:30)

وَوَصَّىٰ بِهَا إِبْرَاهِيمَ بْنِهِ وَيَعْقُوبُ يَا بَنِي إِنَّ اللَّهَ اصْطَفَى لَكُمُ الدِّينَ فَلَا تَمُونُنَ إِلَّا وَأَنْتُمْ مُسْلِمُونَ

"Na Ibraahiyam akawausia hayo wanawe na [kadhalika] Ya'quwb [akawaambia]: "Enyi wanangu! Hakika Allaah Amekuchagulieni nyinyi Dini; basi msife isipokuwa nyinyi ni Waislamu." (02:132)

ثُمَّ أُوحِيَنَا إِلَيْكَ أَنْ اتَّبِعْ مَلَةَ إِبْرَاهِيمَ حَنِيفًا ۚ وَمَا كَانَ مِنَ الْمُشْرِكِينَ

"Kisha Tukakufunulia Wahy kwamba fuata imani ya Ibraahim iliyo safi na kutakasika na hakuwa mionganini mwa washirikina." (16:123)

Ibn Mas'uud (**Radhiya Allaahu 'anh**) ameeleza kuwa Mtume wa Allaah (**Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam**) amesema:

"Hakika kila Mtume ana msaidizi katika Mitume na mimi msaidizi

wangu katika wao ni baba yangu na Khaliyl wa Allaah Ibraahiyim." Halafu akasoma:

إِنَّ أُولَئِي النَّاسِ بِإِيمَانِهِمْ لَلَّذِينَ اتَّبَعُوهُ وَهَذَا النَّبِيُّ وَالَّذِينَ آمَنُوا ۖ وَاللَّهُ وَلِيُّ الْمُؤْمِنِينَ

"Hakika watu waliokaribu zaidi kwa Ibraahiyim ni wale waliomfuata, kama mfano wa Nabii huyu na wale walioamini. Na Allaah ni Mlinzi wa Waumini."[\[29\]](#) (03:68)

Ameipokea at-Tirmidhiy.

Abu Hurayrah (*Radhiya Allaahu 'anh*) ameeleza kuwa Mtume wa Allaah (*Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam*) amesema:

"Allaah hatazami miili yenu wala mali zenu; Anatazama nyoyo zenu na matendo yenu."[\[30\]](#)

al-Bukhaariy na Muslim wamepokea kutoka kwa Ibn Mas'uud (**Radhiya Allaahu 'anh**) ambaye ameелеza kuwa Mtume wa Allaah (**Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam**) amesema:

"Nitasimama nikiwangoja kwenye hodhi. Wanaume katika Ummah wangu watanyanyuliwa kwangu na pindi ninapoenda kuwachukua, **watawekwa mbali na mimi ambapo nitasema**: "Ee Mola! Wafuasi wangu!" Kusemwe: "Hakika wewe hujui waliyozusha baada yako."[31]

al-Bukhaariy na Muslim wamepokea kupitia kwa Abu Hurayrah (**Radhiya Allaahu 'anh**) ya kwamba Mtume wa

Allaah (**Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam**) amesema:

"Ninatamani lau tungeliwaona ndugu zetu." **Waseme:** "Ee Mtume wa Allaah! Kwani sisi sio ndugu zako?"

Aseme: "Nyinyi ni Maswahabah zangu. Ndugu zangu ni wale ambao bado hajaja." **Wakasema:** "Ee

Mtume wa Allaah! Vipi utamjua ni katika Ummah wako ambaye bado hajaja?" **Akajibu:** "Mnaonaje lau mtu atakuwa na farasi aliye na doa kati ya farasi weusi, **hatomjua farasi wake?**"

Wakasema: "Ndio, ee Mtume wa Allaah." **Akasema:** "Watakuja wakiwa na madoa [mwanga] kutokana na wudhuu. Nitawaongoja katika hodhi. Hata hivyo kuna wanaume

wataofukuzwa na hodhi yangu siku ya Qiyaamah kama anavyofukuzwa ngamia aliyepotea. Ninawaita, **lakini kutasemwa:** "Walibadilisha baada yako", **kisha niseme:** "Tokomeeni! Tokomeeni!"[32]

Katika al-Bukhaariy imekuja:

"Nitakuwa nimesimama katika umati wa watu. **Pindi nitapowajua atatoka mtu kati yetu na kusema:** "Njooni!" **Niseme:** "Wapi?" **Aseme:** "Ninaapa kwa Allaah! Motoni." **Niseme:** "Wana nini?" **Aseme:** "Waliritadi baada yako." Halafu kuje umati mwingine", na useme hali kadhalika. Amesema (**Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam**):

"Wachache sawa na idadi ya ngamia waliohuru ndio wataifikia." [\[33\]](#)

al-Bukhaariy na Muslim wamepokea kupidia kwa Ibn 'Abbaas (**Radhiya Allaahu 'anhuma**) ya kwamba Mtume (**Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam**) amesema:

"Nitasma kama alivyosema mja mwema:

وَكُنْتَ عَلَيْهِمْ شَهِيدًا مَا دُمْتُ فِيهِمْ ۝ قَلَّمَا تَوَفَّيْتِي كُنْتَ أَنْتَ الرَّقِيبُ عَلَيْهِمْ ۝ وَأَنْتَ عَلَىٰ كُلِّ
شَيْءٍ شَهِيدٌ

"Na nilikuwa juu yao shahidi wakati nilipokuwa nao, lakini uliponichukua juu [mbinguni] Ulikuwa Wewe ndiye Mwenye kuchunga juu yao; na Wewe juu ya kila kitu ni Shahiyd, Mwenye kushuhudia." [\(05:117\)](#)

al-Bukhaariy na Muslim wamepokea kupitia kwa Abu Hurayrah (**Radhiya Allaahu `anh**) ya kwamba Mtume (**Swalla Allaahu `alayhi wa sallam**) amesema:

"Hakuna mtoto isipokuwa huzaliwa katika maumbile. Baada ya hapo wazazi wake ndio humfanya kuwa myahudi, mnaswara au mwabudu moto. Ni kama mfano mnyama mwenye pembe anavyomzaa mnyama mwenye pembe kama yeye. Je, **mtahisi kuwa hana pembe? Kisha Abu Hurayrah akasoma:**

فَطَرَ اللَّهُ الَّتِي فَطَرَ النَّاسَ عَلَيْهَا

"... imani hiyo ndio maumbile Allaah Aliyowaumbia watu [wote]..." (30:30)

Hudhayfah (Radhiya Allaahu 'anh) amesema:

"Watu walikuwa wakimuuliza Mtume wa Allaah (**Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam**) kuhusu mambo ya kheri na mimi nikimuuliza kuhusu mambo ya shari kwa kuchelea yasije kunipata.

Nikasema: "Ee Mtume wa Allaah! Tulikuwa katika Jaahiliyyah na shari na Allaah akatuletea kheri hii. Je, **kuna shari baada ya kheri hii?**" Akajibu: "Ndio." **Nikasema:** "Je, **kuna kheri baada ya shari hiyo?**" Akajibu: "Ndio, na itakuwa na moshi." **Nikamuuliza:** "Ni upi moshi wake?" Akajibu: "Ni watu wenye kufuata isiyokuwa njia yangu. Kuna mambo utayokubaliana nayo na mengine utayapinga."

Nikasema: "Kuna shari baada ya kheri hiyo?" Akasema: "Ndio, fitina ya upofu na walinganizi katika milango ya Motoni. Yule mwenye kuwaitikia wanamtupa humo." **Nikasema:** "Ee Mtume wa Allaah! Tueleze nao."

Akasema: "Ni watu wanaotokamana na sisi na wanazungumza lugha yetu."

Nikauliza: "Unaniamrisha nini nikikutana na hilo?" Akasema: "Shikamana na mkusanyiko wa waislamu na kiongozi wao."

Nikasema: "Vipi kukiwa hakuna mkusanyiko wala kiongozi?"

Akasema: "Jiepushe na hayo makundi yote hata kama utahitajia kuuma mzizi wa mti mpaka yakufikie mauti." [\[34\]](#)

Ameipokea al-Bulkhaariy na Muslim ambaye amezidisha:

"Kuna nini baadaye?" Akasema:

"Kisha atajitokeza ad-Dajjaal.

Atakuwa na mto na moto.

Atayetumbukia kwenye moto wake itamuwajibikia kulipwa ujira wake na madhambi yake kufutwa. Na yule mwenye kutumbukia kwenye pepo yake itamuwajibikia kuadhibiwa."

Nikasema: "Kuna nini baadaye?"

Akasema: "Halafu kunakuja

Qiyaamah."[\[35\]](#)

Abul-'Aaliyah amesema:

"Jifunzeni Uislamu. Mtapojifunza, msiupe mgongo. Shikamaneni na njia iliyonyooka, kwani hakika ndio

Uislamu. Msende kinyume na njia kuliani na kushotoni. Shikamaneni na Sunnah za Mtume wenu (**Swalla Allaahu `alayhi wa sallam**) na tahadharini na matamanio haya."

Yazingatie maneno haya ya Abul-`Aaliyah - ni matukufu kiasi gani! Tambua zama zake ambapo akitahadharisha matamanio ambayo yule mwenye kuyafuata anakuwa ameupa Uislamu mgongo. Ameufasiri Uislamu kuwa ni Sunnah na khofu yake ilikuwa kwa Taabi'uun mabingwa wasiende kinyume na Quran na Sunnah. **Hapo ndipo itakubainikia maana ya Kauli ya Allaah:**

إذْ قَالَ لَهُ رَبُّهُ أَسْلِمْ ۝ قَالَ أَسْلَمْتُ لِرَبِّ الْعَالَمِينَ

"Pindi Mola Wake Alipomwambia:
"Jisalimishe!" Akajibu:
"Nimejisalimisha kwa [Allaah], Mola
wa walimwengu." (02:131)

na:

وَوَصَّىٰ بِهَا إِبْرَاهِيمَ بَنِيهِ وَيَعْقُوبَ يَا تَبَّيَّ إِنَّ اللَّهَ اصْطَفَى لِكُمُ الْدِّينَ فَلَا تَمُوْذِنُ إِلَّا وَأَنْتُمْ مُسْلِمُونَ

"Na Ibraahiyam akawausia hayo
wanawe na [kadhalika] Ya'quwb
[akawaambia]: "Enyi wanangu!
Hakika Allaah Amekuchagulieni
nyinyi Dini; basi msife isipokuwa
nyinyi ni Waislamu." (02:132)

na:

وَمَنْ يَرْغُبُ عَنْ مَلَأَ إِبْرَاهِيمَ إِلَّا مَنْ سَفَهَ نَفْسَهُ ۝ وَأَقْدَ اصْطَفَيْنَا فِي الدُّنْيَا ۝ وَإِنَّهُ فِي الْآخِرَةِ
لِمِنَ الصَّالِحِينَ

"Na nani atakayejitenga na imani ya
Ibraahiyam isipokuwa anaybeitia nafsi

yake upumbavu? Na kwa yakini
Tumemchagua duniani, naye Aakhirah
ni mionganini mwa [waja] wema."
(02:130)

Izingatie misingi hii mikubwa ambayo
ndio misingi ya misingi na ambayo
watu wameghafilika nayo. Kwa
kuielewa basi itabainika maana ya
Hadiyth katika mlango huu na
mingineyo.

Kuhusiana na yule mwenye kuisoma
sawa hii na mingineyo na huku
anajiaminisha kuwa hayawezi kumfika
na anafikiria kuwa yanawahu su watu
waliokuwepo hapo kale wakatokomea,
basi Allaah yuwasema:

أَفَمُؤْمِنُوا مَكْرُ اللَّهِ ؟ فَلَا يَأْمُنُ مَكْرُ اللَّهِ إِلَّا الْقَوْمُ الْخَاسِرُونَ

"Je, wameaminisha mipango ya Allaah? Basi hawaaminishi mipango ya Allaah isipokuwa watu wenye kukhasirika." (07:99)

Ibn Mas'ud (Radhiya Allaahu 'anh) amesema:

"Siku moja Mtume wa Allaah (**Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam**) alitupigia msitari kwenye ardhi kisha akasema: "Hii ni njia ya Allaah." Halafu akapiga vimisitari kuliani na kushotoni kisha akasema: "Hivi ni vichochoro. Kuna Shaytwaan mwenye kuita kwenye kila kichochoro." Halafu akasoma:

وَأَنَّ هَذَا صِرَاطٌ مُسْتَقِيمًا فَلَيَتَّبِعُوهُ ۝ وَلَا تَنْتَهُوا السُّبُلَ فَتَفَرَّقَ بِكُمْ عَنْ سَبِيلِهِ ۝ ذَلِكُمْ وَصَاعِدُكُمْ بِهِ لَعَلَّكُمْ تَتَّقَوْنَ

“Hii ndio njia Yangu, [njia]

iliyonyooka; basi ifuateni na wala msifuate vichochoro [vinginevyo]; vitakufarikisheni na njia Yake!" Hivyo ndivyo Alivyokuusieni (**Allaah**) kwayo mpate kuwa na taqwa." **[36]** (06:153)

12. Ugeni wa Uislamu na ubora wa wageni

Allaah (**Ta'ala**) amesema:

فَلَوْلَا كَانَ مِنَ الْفَرُّوْنَ مِنْ قَبْلِكُمْ أَوْ لَوْ بَقَيَّةٌ يَهُمُونَ عَنِ الْفَسَادِ فِي الْأَرْضِ إِلَّا قَلِيلًا مِمَّنْ أَنْجَيْتَا
مِنْهُمْ ۝ وَاتَّبَعُ الدِّينَ ظَلَمُوا مَا أَنْتُ فُؤَا فِيهِ وَكَانُوا مُجْرِمِينَ

"Basi kwanini hawakuweko katika karne za kabla yenu, watu weledi wanakataza ufisadi katika ardhi isipokuwa wachache kati ya Tuliowaokoa mionganini mwao! Na wale waliodhulumu wakafuata [anasa] walizostareheshwa nazo na wakawa

wahalifu." (11:116)

Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anh) ameeleza kuwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

"Uislamu ulianza kama kitu kigeni na utarudi kuwa mgeni kama jinsi ulivyoanza - Twubaa kwa wageni!"[37]

Ameipokea Muslim.

Ahmad amepokea kupitia kwa Ibn Mas'uud (Radhiya Allaahu 'anh) ya kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) aliulizwa:

"Ni kina nani wageni?" Akajibu: "Ni watu wachache katika makabila."[38]

Katika upokezi mwingine imekuja:

"Wageni ni wale wanaotengeneza pale wanapoharibika watu."[\[39\]](#)

Ahmad amepokea kupitia kwa Sa'ad bin Abiy Waqqas kwa muundo:

"Twuubaa kwa wageni siku ambayo watu wameharibika!"

at-Tirmidhiy amepokea kupitia kwa Kathiyr bin 'Abdillaah, kutoka kwa baba yake, **kutoka kwa babu yake kwa muundo:**

"Twuubaa kwa wageni wenye kutengeneza yale waliyoharibu watu katika Sunnah zangu!"[\[40\]](#)

Abu Umayyah amesema:

"Nilimuuliza Abu Tha'labah al-Khushaniy (**Radhiya Allaahu 'anh**) juu ya Aayah:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا عَلَيْكُمْ أَنفُسُكُمْ ۝ لَا يَضُرُّكُمْ مَنْ ضَلَّ إِذَا هُنَّتَّبِينَ

"Enyi mlioamini! Ni juu yenu [majukumu ya] nafsi zenu.

Hawakudhuruni waliopotoka, ikiwa mmeongoka." (05:105)

Akajibu: "Ninaapa kwa Allaah ya kwamba mimi mwenyewe nilimuuliza nayo mtu mjuzi; nilimuuliza Mtume wa Allaah na akasema: "Mtaamrishana mema na kukatazana maovu. Pindi mnapoona choyo inayotiiwa, matamanio yanayofuatwa, dunia inayopewa kipaumbele na jinsi kila mmoja anavyopendekeza maoni yake, shikamana na nafsi yako na uachane na

‘Awwaam. Mbele yenu kunakuja masiku ambayo mwenye subira ni kama mfano wa aliyeshika kaa [la moto] na mtendaji mwenye kutenda kama nyinyi analipwa ujira wa wanaume khamsini." **Tukasema:** "Katika sisi au katika wao?" Akasema: "Katika wao."**[41]**

Ameipokea Abu Daawuud na at-Tirmidhiy.

Ibn Wadhdhwaah amepokea maana kama hiyo kutoka kwa Ibn ‘Umar (**Radhiya Allaahu ‘anhumaa**) kwa muundo:

"Baada yenu kunakuja masiku ambayo yule aliyeshikamana na yale mnayofanya nyinyi hii leo analipwa

ujira wa wanaume khamsini katika nyinyi."

Kisha akasema: "Muhammad bin Sa'iyd ametueleza: Asad ametueleza: Sufyaan bin 'Uyaynah ametueleza, kutoka kwa Aslam al-Baswriy, kutoka kwa Sa'iyd, ndugu wa al-Hasan, kutoka kwa Mtume (**Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam**). **Nikamwambia Sufyaan:** "Haya yanatoka kwa (**Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam**)?" Akasema: "Ndio." Amesema (**Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam**):

"Hii leo mko katika ushahidi kutoka kwa Mola Wenu, mnaamrisha mema, mnakataza maovu na mnapigana Jihaad kwa ajili ya Allaah na

hamjasibiwa na vilevi viwili ambacho ni kilevi cha ujinga na kilevi cha kupenda maisha. Hata hivyo mtakuja kubadilika muache kuamrisha mema, kukataza maovu, kupigana Jihaad kwa ajili ya Allaah na mtasibiwa na vilevi viwili. Siku hiyo yule mwenye kushikamana na Kitabu na Sunnah analipwa ujira khamsini." [Wakasema](#): "Katika sisi?" Akasema: "Hapana. Katika nyinyi." [\[42\]](#)

Amepokea kwa mlolongo wa wapokezi kupitia kwa al-Mu'aafiri ambaye ameeleza kuwa Mtume wa Allaah ([Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam](#)) amesema:

"Twuubaa kwa wageni wenye
kushikamana na Kitabu pindi
kinapoachwa na wanaitendea kazi
Sunnah pindi inapozimwa!"[\[43\]](#)

-

13. Matahadharisho ya Bid'ah

al-'Irbaadhw bin Saariyah (**Radhiya Allaahu 'anh**) amesema:

"Mtume wa Allaah (**Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam**) alitutolea mawaidha makali ambayo yalizitikisa nyoyo zetu na macho yetu yakatiririka machozi.

Tukasema: "Ee Mtume wa Allaah! Ni kana kwamba ni mawaidha ya kutuaga; tuusie!" Akasema:

"Ninakuusieni kumcha Allaah (**'Azza**

wa Jall) na kusikiliza na kutii hata kama mtataliwa na mtumwa. Hakika yule atakayeishi katika nyinyi basi atakuja kuona tofauti nyingi. Hivyo basi, shikamaneni na Sunnah zangu na Sunnah za makhaliyfah wangu watakasifu waongofu baada yangu. Ziumeni kwa magego. Tahadharini na mambo ya kuzua, kwani hakika kila Bid'ah ni upotevu."[44]

at-Tirmidhiy amesema:

"Hadiyth ni Hasan na Swahiyh."

Hudhayfah (*Radhiya Allaahu 'anh*) amesema:

"Kila 'ibaadah ambayo hawakuabudu kwayo Maswahabah wa Muhammad

(Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) basi na nyinyi msiabudu kwayo. Wale wa kwanza hawakuwapa wa mwisho la kusema. Mcheni Allaah, enyi wanazuoni, na chukueni njia ya waliokuwa kabla yenu."[\[45\]](#)

Ameipokea Abu Daawuud.

ad-Daarimiy amesema: "al-Hakam bin Mubaarak ametueleza: 'Amr bin Yahyaa ametueleza: Nilimsikia baba yangu akieleza kutoka kwa baba yake ambaye amesema:

"Tulikuwa tukikaa nje ya mlango wa 'Abdullaah bin Mas'eed ([Radhiya Allaahu 'anh](#)) kabla ya Fajr na anapotoka tunaenda naye mpaka msikitini. Siku moja akatujia Abu

Muusa al-Ash'ariy (Radhiya Allaahu 'anh) na kusema: "Abu 'Abdir-Rahmaan ameshakujieni?" Tukasema: "Hapana." Akakaa na sisi mpaka alipotoka. Alipotoka sote tukasimama.

Abu Muusa akamwambia: "Ee Abu 'Abdir-Rahmaan! Hivi karibuni nimeona msikitini kitu nimechokipinga na ilikuwa ni kitu cha kheri tu."

Akasema: "Ni kipi?" Akasema: "Ukiishi utakiona. Msikitini nimewaona watu wamekaa mzunguko wakisubiri swalah. Katika kila mzunguko kuna mtu na kwenye mikono yao wana vijiwe vidogo vidogo.

Anasema: "Semeni: "Allaahu Akbar" mara mia", wanafanya hivo.

Kisha anasema: "Semeni: "Laa ilaaha illa Allaah" mara mia", wanafanya

hivo. **Kisha anasema:** "Semeni: "Subhaana Allaah" mara mia", wanafanya hivo." **Akasema:** "Uliwaambia nini?" Akasema: "Sikuwaambia kitu. Ninasubiri neno lako au amri yako." **Akasema:** "Ungeliwaamrisha wahesabu madhambi yao na kuwadhamini kuwa hakuna chochote katika mema yao kitachopotea." Halafu akaenda na tukafuatana naye. **Alipofika katika mzunguko mmoja miongoni mwa mizunguko ile akasimama na kusema:** "Nini haya ninayoona mnafanya?" Wakasema: "Ee Abu 'Abdir-Rahmaan! Ni vijiwe tu ambavyo tunafanya navyo Takbiyr, Tahliyl na Tasbiyh."

Akasema: "Hesabuni madhambi yenu. Mimi ninakudhaminini hakuna

chochote katika mema yenu kitachopotea. Ee Ummah wa Muhammad! Ole wenu! Ni haraka iliyaje mmeangamia! Hawa hapa Maswahabah wa Mtume wenu (**Swalla Allaahu `alayhi wa sallam**) bado wamejaa, nguo zake hazijaharibika na chombo chake hakijapasuka. Ninaapa kwa yule ambaye nafsi yangu iko Mkononi Mwake ima nyinyi mkono katika dini bora kuliko dini ya Muhammad au mmefungua mlango wa upotevu." **Wakasema:** "Ee Abu `Abdir-Rahmaan! Hatukukusudia jengine isipokuwa kheri tu." **Akasema:** "Ni wangapi wenye kutaka kheri na hawaifiki! Mtume wa Allaah (**Swalla Allaahu `alayhi wa sallam**) ametueleza kuwa kutakuwepo watu wataoisoma

Qur-aan bila ya kuvuka koo zao.
Ninaapa kwa Allaah sijui pengine
wengi wao ndio nyinyi wenyewe."
Kisha akatoka pale akenda zake."
*'Amr bin Salamah amesema: "Tuliona
wengi katika wao wakishirikiana na
Khawaarij siku ya Nahrawaan."* [\[46\]](#)

Allaah ndiye Mwenye kutakwa msaada
na Mwenye kutegemewa. Swalah na
salaam zimwendee kiongozi wetu
Muhammad, ahli zake na Maswahabah
zake wote.

[\[1\]](#) al-Bukhaariy (2268).

[2] al-Bukhaariy (876) na Muslim (855).

[3] al-Bukhaariy katika "al-Adab al-Mufrad" (1/108).

[4] Ibn-ul-Mubaarak katika "az-Zuhd" (1/21), Ahmad katika "az-Zuhd" (1/196) na Abu Nu'aym katika "Hilyat-ul-Awliyaa'" (1/252).

[5] Ahmad katika "az-Zuhd" (137) na Abu Nu'aym katika "Hilyat-ul-Awliyaa'" (1/211).

[6] al-Bukhaariy (2697) na Muslim (1718).

[7] Muslim (1718).

[8] al-Bukhaariy (7280).

- [9] al-Bukhaariy (6882).
- [10] al-Bukhaariy (7282).
- [11] al-Bid'ah, uk. 61-62.
- [12] al-Bukhaariy (4777) na Muslim (102).
- [13] al-Bukhaariy (6484) na Muslim (41).
- [14] Ahmad (3/5), Ibn Hibbaan (1/376) na al-Haakim (4/643).
- [15] Ahmad (4/114)
- [16] Ahmad (3/387), ad-Daarimiyy (436), Abu Ya'laa (4/102) na wengineo.

[17] Ahmad (4/130), at-Tirmidhiy (2863), Ibn Hibbaan (14/125), Ibn Khuzaymah (3/195) na wengineo.

[18] as-Siyaasah ash-Shar'iyyah (1/82).

[19] Ibn Abiy Haatim (3/729), al-Khatwiyb al-Baghdaadiy katika "Taariykh Baghdaad" (7/379) na al-Laalakaa'iy katika "Sharh Usuw'l I'tiqaad Ahl-is-Sunnah wal-Jama'ah" (1/72).

[20] at-Tirmidhiy (2641).

[21] Ahmad (4/102), Abu Daawuud (4597), al-Haakim (1/218) na at-Twabaraaniy (19/376). Ni Swahiyh

kwa mujibu wa al-Albaaniy katika
”Dhwilaal-ul-Jannah” (2).

[22] al-Bukhaariy (3611) na Muslim
(1066).

[23] Muslim (1854).

[24] Muslim (1017).

[25] Muslim (2674).

[26] Muslim (1067).

[27] al-Bukhaariy (5990) na Muslim
(215).

[28] al-Bukhaariy (5063) na Muslim
(1401).

[29] at-Tirmidhiy (2995), al-Bazaar
(5/345) na al-Haakim (2/320).

[30] Muslim (2564).

[31] al-Bukhaariy (7049) na Muslim (2297).

[32] Muslim (249).

[33] al-Bukhaariy (6587).

[34] al-Bukhaariy (3606) na Muslim (1847).

[35] `Abdur-Razzaaq katika "al-Muswannaf" (11/367), al-Marwaziy katika "as-Sunnah", uk. 13, al-Laalakaa'iy katika "Sharh Usuwil I'tiqaad Ahl-is-Sunnah wal-Jamaa'ah (1/56) na Abu Nu'aym (2/218).

[36] an-Nasaa’iy (6/343), Ahmad (1/435), ad-Daarimiyy (202) na al-Bazzaar (57113).

[37] Muslim (145).

[38] Ahmad (1/398).

[39] Zawaa’id-ul-Musnad (4/73).

[40] at-Tirmidhiy (2630) ambaye amesema: ”Hadiyth ni Hasan na Swahiyh.”

[41] Abu Daawuud (4341), at-Tirmidhiy (3058) na Ibn Maajah (4014).

[42] al-Bid’ah, uk. 133.

[43] al-Bid’ah, uk. 122.

[44] Abu Daawuud (4607), at-Tirmidhiy (2676) na Ibn Maajah (34). Ni Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "al-Irwaa'" (2455).

[45] Ibn-ul-Mubaarak katika "az-Zuhd", uk. 16, al-Marwaziy katika "as-Sunnah" (1/30) na Ibn Abiy 'Aasim katika "as-Sunnah" (1/90).

[46] ad-Daarimiyy (204), Bahshal katika "Taariykh Waaswit" na al-Khatwiyb al-Baghdaadiy katika "Taariykh Baghdaad" (12/162).